



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2022 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2022.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2022.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilionekana kuimaimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) ilionekana kudhoofika. Hali hii iliendelea kuruhusu ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani upande wa magharibi, nyanda za juu kusini magharibi pamoja na maeneo ya kusini. Hali hii ilisababisha maeneo haya kupata mvua zilizoambatana na vipindi vya ngurumo za radi. Joto la bahari upande wa mashariki mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani wakati kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la juu kidogo ya wastani. Joto la bahari kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilikuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani na hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea magharibi mwa nchi yetu. Kwa ujumla mifumo ya hali ya hewa iliyotajwa hapo juu, iliendelea kusababisha mvua zilizoambatanana ngurumo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, nyanda za juu kusini magharibi na magharibi mwa nchi yetu.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2022.

Viashiria vya hali ya hewa tajwa hapo juu vilipelekea baadhi ya maeneo ya nchi kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi hususan katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria, nyanda za juu kusini magharibi, kusini pamoja na maeneo ya magharibi mwa nchi. Hata hivyo maeneo mengine ya nchi yalipata vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2022

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2022

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia)

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika na kuruhusu ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika maeneo ya magharibi, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa huku ikichagiza upatikanaji wa mvua zitakazoambatana na ngurumo katika maneo haya. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa mashariki mwa bahari ya Hindi na upande wa kusini magharibi mwa bahari ya Hindi kunatarajiwa kuwa na joto la juu ya wastani. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Kongo kuelekea magharibi mwa nchi yetu. Kwa ujumla mifumo ya hali ya hewa hapo juu, inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa wa mvua zitakazoambatana na ngurumo kwa baadhi ya maeneo ya magharibi, nyanda za juu kusini-magharibi, kusini pamoja na ukanda wa Ziwa Victoria.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2022.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa hususani katika nusu ya pili ya dekad.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,): Vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache vinatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache vinatarajiwa.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa hususani katika nusu ya pili ya dekad.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz